NIPASHE UK 15.

# Taasisi yahimiza matumizi chanjo za ndani mifugo

**Na Elisante John,** SINGIDA

TAASISI ya Chanjo ya Mifugo Tanzania (TVI) iliyoko Kibaha mkoani Pwani, imewataka wafugaji, kutumia chanjo inayotengenezwa na viwanda vya ndani, ili kukabiliana na vita ya kiuchumi, yenye lengo la kupunguza wingi wa mifugo.

Meneja wa TVI, iliyo chini ya Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Dk. Charles Mayenga, alisema hayo juzi mkoani hapa juu ya uwapo wa chanjo bandia ya matone (TEMEVAC 1-2) ya kumkinga kuku dhidi ya ugonjwa wa mdondo.

Dk. Mayenga alikutana na wafugaji, wataalamu, wafanyabiashara na wamiliki wa maduka ya pembejeo za mifugo kwenye ukumbi wa chuo cha VETA mjini hapa ili kuwapatia elimu ya namna ya kuitambua chanjo bandia ya TEMEVAC 1-2.

Mtaalamu huyo kutoka TVLA inayomiliki kiwanda cha serikali cha kutengeneza chanjo ya mifugo, kilichoko Kibaha mkoani Pwani, alisema kuna baadhi ya watu wameingiza nchini chanjo hiyo ili kuhujumu soko la kuku wa Singida.

"Kama mnakumbuka, chanjo ya matone ilifanyiwa utafiti hapa Singida na imefanikiwa katika kudhibiti ugonjwa wa mdondo au kideri kwa kuku... sasa hivi ipo dawa kama hiyo, inafanana na inayozalishwa na kiwanda cha serikali," alisema.

Dk.Mayenga aliwataka washiriki kuwa makini na chanjo hiyo, kutokana na mwonekano wake ulivyo kwa macho ukionesha maandishi yakiwa hayasomeki vizuri, wakati ile ya serikali yapo kwenye mpangilio mzuri na yanasomeka vyema.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, mmiliki wa duka la dawa, Dk. William Mafwere na Ester Munuo, walipongeza juhudi za serikali kwa kuwapatia elimu ya kutambua chanjo hiyo feki, jambo litakalolinda kazi zao na za wafugaji pia.

TVLA hutengeneza aina saba za chanjo, ikiwamo ya mdondo/kideri (TEMEVAC), homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP), homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP), Kimeta (Anthrax), kimeta na chambavu (Tecoblax), chambavu (Blackquarer) na kutupa mimba (Brucellosis5-19.



fikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

imemkuta na hatia kwa kuwa mshitakiwa alikutwa na baadhi ya vitu alivyoiba ikiwemo telev-

mlango wa nyumba ya Rukia Magere na kuingia ndani.

Katika mashitaka ya pili,

goni mwa walinzi shirikishi na kumtaarifu kuwa mwizi aliyeiba vitu vyake tayari amekamatwa.

saa 5:00 usiku Bwiru Kata y Ilemela polisi mata Donard Kilimahewa a tuhuma za k cha sheria.

Katika tu Mutafungwa huu muda w mtaa huohuo walimkamat wa Kitangiri tuhuma za k vitendo vya mond na Las

Watuhum na watafikish iwezekanavy

HABARI LEO UK 20.

# Waliogawana mifugo ya watuhumiwa matatani

**Na Frank Aman, Simiyu**

JESHI la Polisi mkoani Simiyu linawashikilia watu 10 wakiwemo wazee wa kimila maarufu kama Ndagashida na viongozi wa ulinzi wa jadi maarufu sungusungu kwa tuhuma za kuchukua mifugo kwenye familia za watuhumiwa wa kesi ya mauaji na kugawana.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mkoani humo, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Simiyu, Blasious Chatanda amesema Februari 2023 kulitokea tukio la mauaji ya mfanyabiashara, William Fumbuka (39) katika Kijiji cha Bukundi, wilayani Meatu.

Chanzo cha kifo chake kilibainika kuwa kulikuwepo na mgogoro wa umiliki wa ardhi inayokadiriwa kufikia ekari 2,500 ambayo ilielezwa kuwa Fumbuka alizitumia kuzikodisha.

Kamanda Chatanda alisema baada ya kutokea kwa tukio hilo walifanikiwa kuwakamata watuhumiwa sita na kuwafikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Meatu ndipo viongozi hao wakarudi na kuchukua mifugo katika familia hizo na kugawana kitendo ambacho ni kinyume na sheria.

"Kutokana na kuwepo kwa mgogoro huo katika familia hiyo, watuhumiwa walipanga mipango ya kumuua Fumbuka na walitekeleza tukio hilo na hadi sasa tayari watuhumiwa wa tukio hilo wako mikononi mwa Jeshi la Polisi tayari kwa taratibu za kuwafikisha mahakamani zikiendelea," alisema.



## ya matibabu bila malipo

a

o

malipo,
mfuko
a kwa
shauri,"

fedha
napato
vapatia
liobaki
ya ya

ote wa
ekeleza
bulisho
e wote
aslo na



la

il 21,

kiana
ngozi
rmila
i na
zi wa
eleza

hadili
zima

UHURU UK5.

# Halmashauri zatakiwa kutunga sheria kuzuia uswagaji mifugo

HALMASHAURI nchini, ambazo hadi sasa hazijatunga sheria ndogo za kuzuia uswagaji mifugo, zimeelekezwa kufanya hivyo mara moja.

Maelekezo hayo, yalitolewa bungeni jijini hapa jana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, David Silinde, alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Naghenjwa Kayoboka.

Mbunge huyo, alitaka kujua lini serikali itaweka katazo la kisheria la kuswaga mifugo kuzuia uharibifu wa mazingira.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema usafirishaji wa mifugo, hufanyika chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Sura 156, na Kanuni zake za Udhibiti wa Usafirishaji wa Wanyama na Mazao ya Wanyama, GN 28 za mwaka 2007.

Alieleza kuwa, usafirishaji wa mifugo kutoka wilaya moja kwenda nyingine, hufanyika baada ya mifugo kukaguliwa na wataalamu na kupatiwa kibali cha kusafirishwa.

Aidha, Waraka wa Rais Na. 1 wa Mwaka 2002, uliziagiza Serikali za Mitaa nchini, kutunga sheria ndogo kuzuia uswagaji wa mifugo.

"Kwa maelezo hayo hapo juu, inathibitisha kwamba, sheria ipo. Hivyo basi, wafugaji wanahimizwa kuzingatia Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Sura 156 na Sheria ndogo zilizopo ndani ya halmashauri zao zinazozuia uswagaji wa mifugo.

"Pia, nitumie fursa hii kuzielekeza halmashauri ambazo hadi sasa hazijatunga sheria ndogo za kuzuia uswagaji mifugo, zifanye hivyo mara moja," alisisitiza.

Wakati huo huo, serikali imesema kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi, inatekeleza mikakati mbalimbali kuhakikisha wakulima wakiwemo wa zao la vanilla, wanapata soko la uhakika

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema hayo bungeni, jijini hapa jana alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti Maalumu, Bernadetha Mushashu, aliyetaka kujua lini serikali itatafuta soko la uhakika la zao la vanila.

Mavunde alisema serikali kwa kushiriklana na wadau wa sekta binafsi, inatekeleza mikakati mbalimbali kuhakikisha wakulima wakiwemo wa zao la vanilla, wanapata soko la uhakika.

Alilitaja mikakati hiyo kuwa ni kuhamasisha kilimo cha kibiashara kinachozingatia mahitaji ya soko, kushiriki makongamano na maonyesho ya kibiashara na uwekezaji, ujenzi wa miundombinu ya masoko na kuimarisha mifumo ya kielektroniki ambayo itasaidia upatikanaji wa taarifa za masoko.

Alisema kwamba, serikali inahamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uongezaji thamani wa zao la vanilla, kupanua wigo wa soko la zao hilo.

Aidha, wakulima wa vanilla hilo, wanahimizwa kuvuna zikiwa zimekomaa kukidhi mahitaji ya soko.

Pia, alisema wiki mbili zilizopita, wizara hiyo na wadau wa vanilla, walifanya kikao kwa lengo la kuandaa mwongozo utakaokuwa na mfumo wa bei, masoko na uzalishwaji wa vanilla inayohitajika kimataifa.

Alieleza wameuandikia ubalozi wa Tanzania, nchini China, ambako kuna sehemu kubwa ya soko la zao hilo, kuangalia hilo.

# JUKWAA LA UCHUMI



## Klopp furaha tele Liverpool

BAADA ya juzi timu ya Liverpool kuibuka na ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya Leeds United, Kocha Jurgen Klopp, amesema katika mchezo huo kikosi chake kimeonyesha kiwango bora zaidi tangu msimu huu uanze. >>Uk. 14

# PSSSF yajitanua uwekezaji katika kiwanda cha nyama



# PSSSF yajitanua uwekezaji katika kiwanda cha nyama



Meneja Mkuu wa Machinjio ya kisasa ya Nyama Nguru Hills,Eric Cormack akiwaeleza wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania(TEF) hatua za uchinjaji nyama.

NA JOE NAKAJUMO

TANZANIA ni ya pili barani Afrika, kwa kuwa na idadi kubwa ya ng'ombe ikitanguliwa na Ethiopia.

Takwimu za mwaka 2019/20, zinaonyesha kulikuwa na ng'ombe wapatao milioni 34, mbuzi milioni 25 na kondoo milioni tisa.

Nchini Ethiopia, kwa takwimu za mwaka 2022, zinaonyesha kulikuwa na ng'ombe milioni 54, kondoo milioni 26, na mbuzi milioni 24.

Lakini pamoja na Tanzania kuwa na mamilioni ya mifugo, mchango wake katika uchumi ni mdogo.

Ripoti ya utafiti wa uchumi ya mwaka 2020 inaonyesha sekta ya mifugo ilikuwa na mchango wa asilimia 27 katika sekta ya kilimo.

Hata hivyo, kumekuwepo na mwamko miongoni mwa wafugaji na wawekezaji kwamba mifugo na mazao yake kwa lugha ya mtaani ni biashara inayolipa.

Kwa kutambua kwamba biashara ya mifugo ina tija, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma(PSSSF), imeamua kuingia katika uwekezaji wa biashara hiyo.

PSSSF ambayo ni taasisi ya umma imeingia kwenye biashara ya kununua mifugo na kuchinja kwa kufuata utaratibu wa ubia na kampuni binafsi (Public Private Partnership-(PPP)).

> **"Kwa ujumla hakuna kinachotupwa kutokana na wanyama wanaochinjwa, vyote vina soko...**
>
> **Erick Cormack, Meneja wa Kiwanda**

### WABIA WA PSSSF

Wabia wenza wa PSSSF inayomiliki asilimia 39 ya hisa, ni kampuni ya Eclipse LLC-ya nchini Oman, yenye hisa asilimia 46 na kampuni ya Busara ya Tanzania inamiliki asilimia 15 ya hisa.

Wabia hawa watatu wameanzisha shamba la mifugo na kiwanda cha kisasa cha kuchinja nyama, kwa jina la Nguru Hills Ranch and Abattoir,kilichopo wilayani Mvomero Mkoa wa Morogoro.

Jukwaa la Wahariri Tanzania(TEF), ambalo mwishoni mwa mwezi Machi lilifanya mkutano wake wa mwaka wa kitaaluma mjini Morogoro, wanachama wake kwa mwaliko wa PSSSF walitembelea Nguru Hills kuona kazi zinavyofanywa katika kiwanda cha machinjio.

Msafara wa wanaTEF wapatao 100 kwenda Nguru Hills umbali wa kilomita 20 kwa kufuata barabara iendayo Dodoma kutoka stendi kuu ya mabasi ya Msavu, mjini Morogoro,uliongozwa na Meneja Mawasiliano wa PSSSF, James Mlowe na ulipokewa kiwandani na Meneja wa Kiwanda, Eric Cormack.

### TEF WAFIKA KIWANDA CHA NYAMA

Cormack alianza kuutembeza ujumbe wa TEF, huku akieleza kwamba Kampuni ya Nguru Hills ina sehemu mbili.

Sehemu ya kwanza ni shamba (ranch) lenye eneo la hekta 2,428 na uwezo wa kuwepo ng'ombe 10,000 na mbuzi na kondoo 15,000 kwa wakati mmoja.

Meneja alieleza kwamba shamba linatumika kwa kuinenepesha kwa miezi mitatu mifugo wanayoinunua kutoka kwa wafugaji sehemu mbali mbali nchini kabla ya kuchinjwa.

Alisema hatua hiyo imesaidia kwani kila siku ng'ombe anaongzeka kwa kilo moja. Ng'ombe wote wanaonunuliwa na kiwanda ni madume.

### MACHINJIO YA KISASA

Sehemu ya pili ya kampuni ni kiwanda cha kisasa cha machinjio, alisema meneja na kuongeza kwamba kila siku wanachinjwa ng'ombe 100 na mbuzi 1,000.

Akieleza utaratibu unaofuatwa kabla ya ng'ombe hajachinjwa,Meneja alisema ng'ombe anapumzishwa kwa saa 24 kabla ya kuchinjwa na wakati wa mapumziko anapewa chumvi na maji mengi kiasi cha lita 130 za maji kila ng'ombe.

### HATUA ZA UCHINJAJI

Ikifika hatua ya kuchinjwa,mnyama anayechinjwa anaelekezwa 'Kibra' na baadaye hufuata hatua za ukaguzi wa sehemu tatu za mzoga.

Kuna maofisa wa afya wakaguzi nyama watatu wa serikali ambapo kila mmoja ana sehemu yake ya kukagua.

Wa kwanza anakagua kichwa, wa pili anakagua nyama ya ndani ambayo machinjioni hapo wanaiita nyama nyekundu inayojumuisha utumbo, maini, moyo, mapafu na mkaguzi wa tatu anakagua mzoga nzima wa nyama ambayo imetengwa na kichwa na nyama nyekundu.

Baada ya ukaguzi wa afya nyama inawekwa kupozwa kwenye chumba chenye baridi kali digrii 0 hadi 2 na baadaye nyama ikishakatwa vipande vya kilo moja moja, huifadhiwa katika chumba kingine chenye baridi kali chini ya digrii 48.

Cormack alisema Kiwanda cha Nguru Hills kilichowekezwa kwa dola za Marekani milioni 50, kilianza uzalishaji nyama Juni mwaka jana 2022 na kilizinduliwa rasmi Desemba.

Aliwaeleza wanaTEF ambao wakati wote walikuwa wanamsikiliza kwa makini, kwamba nyama inakatwa kwa vipande vya kilo moja moja na kuhifadhiwa kwa ajili ya soko liwe la ndani au nje ya nchi.

### MENEJA AZUNGUMZIA MASOKO

Meneja alisema asilimia 80 ya soko ni la nchi za nje na asilimia 20 ni la ndani ya nchi. Alizitaja baadhi ya nchi ambazo ni soko lao kubwa ni Qatar, ambako mwaka jana wakati wa mashindano ya Kombe la Dunia waliuza nyama nyingi.

Soko lingine ni Oman na katika siku chache zijazo watauza nyama Saudi Arabia,Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE), Malaysia, Indonesia na nyingine.

Kuhusu sehemu zingine za mnyama, Meneja alisema ngozi zinauzwa kwa Kampuni ya ACE Leather na Kiwanda cha



Nyama iliyoandaliwa tayari kwa kukatwa



**Wahariri wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania(TEF) waliotembelea mwishoni mwa Machi mwaka huu Machinjio ya Kisasa ya Nguru Hills, Mvomero,mkoani Morogoro.**

Ngozi cha Karanga, Moshi mkoani Kilimanjaro.

"Kwa ujumla hakuna kinachotupwa kutokana na wanyama wanaochinjwa,vyote vina soko,"alisema Cormack.

Alifafanua kwamba kama wakaguzi wa afya ya mnyama wamegundua ugonjwa basi huteketezwa.

**BEI ANAYOLIPWA MFUGAJI**

Akijibu swali, wafugaji wananufaikaje na kiwanda,Meneja alisema Kiwanda cha Nyama cha Nguru Hills kinanunua ng'ombe kwa wafugaji kwa bei ya sh.3,500 za Tanzania kwa kilo mnyama akiwa hai.

Kigezo kingine ni kwamba Kiwanda - kinanunua ng'ombe wenye umri wa chini ya miaka mitano na wenye wastani wa uzito wa kilo 250.

Cormack alisema bei ya nyama kwa soko la ndani zinatofautiana kutokana na uchakataji wa nyama unaofanyika ambao ni wa kisasa kwa mikato maalumu.

**BEI KWA WATEJA**

Kwa nyama ya ng'ombe kuna wastani wa bei ya sh.16,000 kwa prime cuts na wastani wa Sh.10,000 hadi sh.25,000 kwa mikato ya kawaida(local cuts).

Meneja alisema nyama ya mbuzi na kondoo inauzwa kwa wastani wa sh.11,500.

Cormack alisema Nguru Hills ina jumla ya wafanyakazi wa kudumu 70,na katika siku chache zijazo wataongezeka hadi 250.Lakini mnyororo nzima wa utendaji katika kiwanda unahusisha wafanyakazi 2,000.

Baada ya kutembezwa katika kila hatua kuanzia ng'ombe anapoingizwa kiwandani na kuelekezwa 'Kibra' tayari kuchinjwa hadi ghala la kuhifadhia nyama iliyofungwa kwenye paketi,

**KAMPUNI**

**Wabia wenza wa PSSSF inayomiliki asilimia 39 ya hisa, ni kampuni ya Eclipse LLC- ya nchini Oman, yenye hisa asilimia 46 na kampuni ya Busara ya Tanzania inamiliki asilimia 15 ya hisa.**

wana TEF wakaribishwa chakula.

Hapo ndipo, wenye uroho wa kula nyama walipokomeshwa.. Chakula kilikuwa ni nyama choma na ndizi choma tu.w

Tanzania imekuwa na utajiri wa mifugo mingi hasa ng'ombe,lakini uchangiaji wake katika uchumi binafsi wa mfugai mmoja mmoja na taifa ni mdogo.

Hata inatia moyo kwamba baadhi ya wafugaji nchini wameanza kuwa na mwamko wa kufuata ufugaji wa kisasa utakaowaletea tija katika kufanya biashara hiyo.

Katika kusaidia kukuza biashara ya mifugo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alifanya ziara nchini Italia hivi karibuni, ambako alikutana na wadau wa sekta ya mifugo.

Waziri aliwaeleza wadau kwamba,. hivi sasa serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imedhamiria kubadilisha mfumo wa uzalishaji wa sekta za mifugo na uvuvi, kutoka kufanya shughuli zao za kiasili na kujiendesha kibiashara,kuongeza uzalishaji wake.

Ulega aliwaeleza wadau kwamba, serikali ya Tanzania ingependa kupata wawekezaji mahiri katika sekta ya mifugo, hususan biashara ya nyama kwa kushirikiana na Kampuni ya Ranchi za Taifa(NARCO).

Wakati wa ziara, Waziri Ulega alikutana na viongozi wa taasisi ya Benki ya Uwekezaji ya Italia,Shirika la Umoja wa Mataifa la Viwanda (UNIDO) COGEMAT Slaughtering and Meat Technology.

**WALA NYAMA HADI KUKINAI**

Na hakukuwa na kipimo maalumu, isipokuwa mpakuaji anakulundikia tu minyama na ndizi mpaka utakapostuka na kusema "eeh basi inatosha," na kama ni mtumiaji pilipili, kiliwekwa 'kidumu' cha pilipili na kachumbari, unaiweka juu ya kichuguu cha nyama.

Samahani msomaji wangu kama udenda utakutoka kwa uchu baada ya kusoma aya hiyo.

Tukumbuke huu ulikuwa bado ni wakati wa mfugo wa Kwaresima kwa Wakristo na Ramadhan kwa Waislamu. Wale waliokuwa wamefunga walifungashiwa 'mizigo' yao ya nyama waendelee nayo wakati wa kufuturu.

Hiyo ndio ilikuwa ziara ya mafunzo ya wanaTEF Nguru Hills kwa ufadhili na maandalizi ya PSSSF chini ya usimamizi wa Meneja Mawasiliano James Mlowe, siku ile ya Ijumaa ya Machi 31, mwaka huu.

Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile na Meneja Mawasiliano PSSSF, Mlowe walisisitiza kuendelea kukuza na kuimarisha ushirikiano baina ya taasisi hizi mbili

**(Mawasiliano ya Mwandishi WhatsApp 0784291434 email nakajumoj@gmail.com)**



**Wahariri wakitembelea kiwanda cha nyama.**